SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**


**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza Kutumika.

2. Marekebisho ya Sheria mbalimbali.

**SEHEMU YA PILI**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI NA UHIFADHI WA RASILIMALI ZA MISITU, NAM. 10 YA 1996**

3. Kusomwa.

4. Marekebisho ya kifungu cha 35.

**SEHEMU YA TATU**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA UVUVI, NAM. 7 YA 2010**

5. Kusomwa.

6. Marekebisho ya kifungu cha 3.

7. Kufutwa kwa kifungu cha 12.

**MAREKEBISHO YA SHERIA YA ELIMU, NAM. 6 YA 1982**

8. Kusomwa.

9. Marekebisho ya kifungu cha 17.

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA AFYA YA JAMII NA MAZINGIRA, NAM. 11 YA 2012

10. Kusomwa.

11. Marekebisho ya kifungu cha 30.

12. Kufutwa kwa kifungu cha 52.

13. Kufutwa na kuandikwa upya kwa kifungu cha 58.

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UCHAGUZI, NAM. 4 YA 2018

14. Kusomwa.

15. Marekebisho ya kifungu cha 53.

## SEHEMU YA SABA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA, NAM. 7 YA 2014

16. Kusomwa.

17. Marekebisho ya kifungu cha 2.

18. Kuongezwa kifungu kipya cha 12A.

19. Marekebisho ya kifungu cha 18.

20. Marekebisho ya kifungu cha 20.

21. Marekebisho ya kifungu cha 22.

22. Marekebisho ya kifungu cha 24.

23. Marekebisho ya kifungu cha 25.

24. Marekebisho ya kifungu cha 26.

25. Kuongezwa kifungu kipya cha 26A.

26. Kuongezwa kifungu kipya cha 26B.

27. Kuongezwa kifungu kipya cha 26C.

28. Marekebisho ya kifungu cha 39.

29. Kuongezwa kifungu kipya cha 39A.

30. Marekebisho ya kifungu cha 41.

31. Marekebisho ya kifungu cha 42.

32. Marekebisho ya kifungu cha 43.

33. Marekebisho ya kifungu cha 47.

34. Marekebisho ya kifungu cha 57.

35. Marekebisho ya kifungu cha 70.

36. Marekebisho ya kifungu cha 72.

37. Marekebisho ya kifungu cha 75.

38. Kuongezwa kifungu kipya cha 86A.

39. Kuongezwa kifungu kipya cha 86B.

40. Kuongezwa kifungu kipya cha 86C.

41. Marekebisho ya Jadweli la Kwanza.

## SEHEMU YA NANE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA (UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI) MAFUTA NA GESI ASILIA NAM. 6 YA 2016

42. Kusomwa.

43. Marekebisho ya kifungu cha 17.

**SHERIA NAM. 14 YA 2020**

**NIMESAINI**

**{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

3 Julai, **2020**

# SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali mbali, 2020 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

Marekebisho ya sheria mbali mbali.

**2.** Sheria zilizotajwa katika sehemu mbalimbali za Sheria hii zinarekebishwa kwa namna zinavyoelezwa katika sehemu husika.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI NA UHIFADHI WA RASILIMALI ZA MISITU, NAM. 10 YA 1996

Kusomwa.

**3.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usimamizi na Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu, Nam.10 ya 1996, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama “Sheria Mama”.

Marekebisho ya kifungu cha 35.

**4.** Kifungu cha 35 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (3) kama ifuatavyo:

"(3) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Msimamizi wa Misitu katika uanzishaji wa Kikundi cha Usimamizi wa Misitu ya Jamii:

(a) atashauriana na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika na kuwasilisha mapendekezo kwa Waziri, na

(b) Waziri kabla ya kutoa maamuzi kuhusiana na mapendekezo hayo, atashauriana na Waziri anayehusika na Mamlaka ya Serikali za Mitaa".

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UVUVI, NAM. 7 YA 2010

Kusomwa.

**5.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Uvuvi, Nam. 7 ya 2010, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**6.** Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa katika ufafanuzi maneno: "Ufugaji wa viumbe maji" na "Diko".

Kufutwa kwa kifungu cha 12.

**7.** Kifungu cha 12 cha Sheria Mama kinafutwa.

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA ELIMU, NAM. 6 YA 1982

Kusomwa.

**8.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Elimu, Nam. 6 ya 1982, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 17.

**9.** Kifungu cha 17 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo cha (3) kama ifuatavyo:

"(3) Kwa madhumuni ya elimu ya maandalizi na elimu ya msingi, Waziri atashauriana na Waziri anayehusika na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhusiana na mambo yanayohusiana na kifungu hiki".

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA AFYA YA JAMII NA MAZINGIRA, NAM. 11 YA 2012

Kusomwa.

**10.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Afya ya Jamii na Mazingira, Nam. 11 ya 2012, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 30.

**11.** Kifungu cha 30 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa kifungu kidogo cha (2).

Kufutwa kwa kifungu cha 52.

**12.** Kifungu cha 52 cha Sheria Mama kinafutwa.

Kufutwa na kuandikwa upya kwa kifungu cha 58.

**13.** Kifungu cha 58 cha Sheria Mama kinafutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 58 kama ifuatavyo:

"Taarifa ya maradhi ya kuambukiza.

58 (1) Endapo mmiliki au mtu mwenye dhamana ya chombo chochote wakati chombo hicho kipo katika bandari yoyote ya Zanzibar, atabaini kuwa yumo abiria au mtu yeyote ana maradhi ya kuambukiza au dalili za maradhi ambayo yanaweza kuleta mashaka kwamba ni maradhi ya kuambukiza, atampa taarifa Daktari na masharti yafuatayo yatafuatwa:

(a) Daktari anayeshiriki au aliyeitwa kumtembelea mgonjwa, atakapotambua kuwa mgonjwa huyo anasumbuliwa na maradhi ya kuambukiza au yanayodhaniwa yanaambukiza, atapeleka taarifa kwa Daktari Dhamana wa Wilaya inayoelezea jina na jinsia ya mgonjwa, hali ya chombo, vyanzo na sababu ya maradhi ambayo, kwa mawazo ya daktari huyo, mgonjwa huyo anasumbuliwa au anadhaniwa kuwa anasumbuliwa;

(b) Mgonjwa yeyote au jamaa wa mgonjwa ambaye amefanyiwa uchunguzi au anadhaniwa kupata maradhi ya kuambukiza atajulishwa na daktari na atalazimishwa kufuata maelekezo aliyopewa na hatua zilizochukuliwa na Daktari;

(c) Mtumiaji au mmiliki wa chombo, mara atakapojuwa kuwa mgonjwa anasumbuliwa na maradhi ya kuambukiza au anadhaniwa kuwa anasumbuliwa na maradhi ya kuambukiza, apeleke taarifa inayohusiana na maradhi hayo kwa Afisa Afya wa Bandari.

(2) Mtu anayehitajika na kifungu hiki kupeleka taarifa au cheti na akashindwa kupeleka vitu hivyo, atakuwa ni mkosa na atalipa faini isiyopungua Shilingi Laki Tano au kifungo kwa muda wa miaka mitatu au vyote viwili faini na kifungo.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, Bandari inajumuisha Bandari yoyote ya Zanzibar, iliyo rasmi au isiyokuwa rasmi".

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UCHAGUZI, NAM. 4 YA 2018

Kusomwa.

**14.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Uchaguzi, Nam. 4 ya 2018, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 53.

**15.** Kifungu cha 53 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa kifungu kidogo cha (4).

## SEHEMU YA SABA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA, NAM. 7 YA 2014

Kusomwa.

**16.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Nam.7 ya 2014, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**17.** Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza maneno mapya katika ufafanuzi kwa mpangilio wa kiherufi kama ifuatavyo:

"kilimo" maana yake ni mazao yanayolimwa katika ardhi au vitalu ardhini, misitu na rasilimali zinazotokana na mazingira yoyote ya uoteshaji;

"ufugaji wa viumbe maji" maana yake ni kitendo cha kulea au kukuza samaki au mazao ya baharini katika mazingira ya maji;

"mazao ya baharini" maana yake ni aina zote za mazao zinazopatikana baharini;

"diko" maana yake ni eneo la fukwe katika kijiji ambalo kwa kawaida hutumiwa na wavuvi kushushia samaki au kuegesha vyombo vya uvuvi baada ya kurejea kutoka katika shughuli zao za uvuvi vilevile hulitumia eneo hilo kwa matengenezo ya vyombo vya uvuvi na kufanya shughuli za utafiti zikiwemo ukusanyaji wa taarifa pamoja na shughuli nyengine zilizoidhinishwa na kamati za wavuvi;

Kuongezwa kifungu kipya cha 12 A.

**18.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 12A mara baada ya kifungu cha 12 kama ifuatavyo:

"Uwezo wa Serikali Kuu kuhusisha na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

12A. Bila ya kujali uwezo wa jumla wa Serikali Kuu, kwa kuhusisha na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Serikali Kuu itakuwa na nguvu za kuingia maamuzi au amri za Mamlaka ya Serikali za Mitaa ikiwa maamuzi au amri hizo zipo kinyume na:

(i) sheria za Zanzibar;

(ii) maslahi ya umma;

(iii) usalama wa taifa na miongozo ya Serikali; au

(iv) sababu nyengine yoyote ambayo Serikali itaona inafaa".

Marekebisho ya kifungu cha 18.

**19.** Kifungu cha 18 (2) cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta aya ya (b) na kuwekwa badala yake aya ya (b) mpya kama ifuatavyo:

"(b) Naibu Meya ambaye atachaguliwa na Madiwani wa Baraza la Jiji kutoka miongoni mwa Madiwani wa Manispaa, isipokuwa kwamba pale ambapo Meya atatoka katika Baraza moja la Manispaa, Naibu Meya atatoka katika Baraza la Manispaa nyengine".

(b) kufuta aya ya (d) na kuwekwa badala yake aya ya (d) mpya kama ifuatavyo:

"(d) Madiwani wengine watano kutoka kila Manispaa ambao wataunda Baraza la Jiji kuziwakilisha Manispaa zao, angalau wawili kati yao wawe wanawake".

(c) kufuta aya ya (e) na kuwekwa badala yake aya ya (e) mpya kama ifuatavyo:

"(e) Madiwani wengine watano ambao watateuliwa na Waziri kwa kuzingatia taaluma zao, elimu au uzoefu kwenye fani za sheria, uchumi, mipango, ualimu, utawala wa umma au fedha, wawili kati yao wawe wanawake".

Marekebisho ya kifungu cha 20.

**20.** Kifungu cha 20 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta aya ya (d) ya kifungu kidogo cha (1) na kuwekwa badala yake aya ya (d) mpya kama ifuatavyo:

"(d) kutakuwa na asilimia arobaini ya viti maalum vya Madiwani wanawake katika kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa baada ya uchaguzi wa Madiwani katika uchaguzi mkuu".

(b) kuongeza aya mpya ya (e) mara tu baada ya aya ya (d) kama ifuatavyo:

"(e) Madiwani wengine watano ambao watateuliwa na Waziri kwa kuzingatia taaluma zao, elimu au uzoefu kwenye fani za sheria, uchumi, mipango, ualimu, utawala wa umma, fedha fani nyengine inayolingana, angalau wawili kati yao wawe wanawake".

Marekebisho ya kifungu cha 22.

**21.** Kifungu cha 22 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta aya (d) ya kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake aya (d) mpya kama ifuatavyo:

"(d) kutakuwa na asilimia arobaini ya viti maalum vya Madiwani wanawake katika kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa baada ya uchaguzi wa Madiwani katika uchaguzi mkuu".

(b) kuongeza aya mpya ya (e) mara tu baada ya aya ya (d) kama ifuatavyo:

"(e) Madiwani wengine watano ambao watateuliwa na Waziri kwa kuzingatia taaluma zao, elimu au uzoefu kwenye fani za sheria, uchumi, mipango, ualimu, utawala wa umma, fedha au fani nyengine inayolingana, angalau wawili kati yao wawe wanawake".

Marekebisho ya kifungu cha 24.

**22.** Kifungu cha 24 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta aya ya (d) ya kifungu kidogo cha (1) na kuwekwa badala yake aya (d) mpya kama ifuatavyo:

"(d) kutakuwa na asilimia arobaini ya viti maalum vya Madiwani wanawake katika kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa baada ya uchaguzi wa madiwani katika uchaguzi mkuu".

(b) kuongeza aya mpya ya (e) mara tu baada ya aya ya (d) kama ifuatavyo:

"(e) Madiwani wengine watano ambao watateuliwa na Waziri kwa kuzingatia taaluma zao, elimu au uzoefu kwenye fani za sheria, uchumi, mipango, ualimu, utawala wa umma, fedha au fani nyengine inayolingana, angalau wawili kati yao wawe wanawake".

Marekebisho ya kifungu cha 25.

**23.** Kifungu cha 25 (1) cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza aya mpya za (d) na (e) mara tu baada ya aya ya (c) kama ifuatavyo:

"(d) kwa kuzingatia mipango ya kitaifa na programu kwa maendeleo ya vijiji na miji, kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi".

"(e) kukuza afya, elimu, huduma za kijamii na utamaduni kwa maisha bora ya watu".

Marekebisho ya kifungu cha 26.

**24.** Kifungu cha 26 cha Sheria Mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (2) mara baada ya kifungu kidogo cha (1) kama ifuatavyo:

"(2) kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Elimu Nam. 6 ya 1982 na amri yoyote ya kiutawala, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kwa kuzihusisha na elimu, zitakuwa na jukumu la jumla la usimamizi na uendeshaji wa skuli za maandalizi na skuli za msingi ikijumuisha:

(i) uandikishwaji wa lazima na mahudhurio;

(ii) upatikanaji wa mazingira bora ya ufundishaji na kujifunza; na

(iii) uajiri wa wafanyakazi.

(b) kuweka namba upya kifungu kidogo cha (2) kuwa kifungu kidogo cha (3) kwa mpangilio wake.

(c) kuifuta aya ya (n) katika kifungu kidogo cha (1)".

Kuongezwa kifungu kipya cha 26A.

**25.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 26A mara baada ya kifungu cha 26 kama ifuatavyo:

"Uanzishwaji wa kamati za skuli.

26A.-(1) Kutakuwa na Kamati ya Skuli katika kila skuli za maandalizi na msingi za Serikali itakayokuwa na muundo ufuatao:

(a) Mwenyekiti ambaye atachaguliwa miongoni mwa wazee au walezi kutoka katika jamii husika;

(b) mjumbe mmoja kutoka katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya eneo ambalo skuli hiyo ipo;

(c) mjumbe mmoja kutoka katika kila shehia ndani ya eneo ambalo skuli hiyo inahudumia ambaye atateuliwa na Sheha husika;

(d) si zaidi ya wajumbe wawili ambao watateuliwa na Mkurugenzi husika wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa;

(e) si zaidi ya wajumbe watatu watakaoteuliwa na wazazi wenyewe;

(f) kiongozi wa serikali ya wanafunzi ya skuli hiyo; na

(g) mwalimu mkuu wa skuli hiyo atakuwa katibu wa Kamati.

(2) Wajumbe wa kamati ya skuli watashika nafasi zao kwa muda wa miaka mitatu, lakini wanaweza kuteuliwa tena.

(3) Kazi, utaratibu na mambo mengine yanayohusiana na hayo chini ya kifungu hiki yatakuwa kama yatakavyoelezwa katika Kanuni".

Kuongezwa kifungu kipya cha 26B.

**26.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 26B mara baada ya kifungu cha 26A kama ifuatavyo:

"Uanzishwaji wa Bodi ya Elimu ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

26B.(1) Kutakuwa na Bodi ya Elimu ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambayo itajumuisha wajumbe wafuatao:

(a) mwenyekiti ambaye atateuliwa na Waziri ambaye atakuwa ni mtu mwenye hadhi na mwenye kustahiwa na watu katika maeneo yanayohudumiwa na skuli na hatokuwa ni mtu kutoka katika Wizara au taasisi yake yoyote;

(b) mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Mkurugenzi husika wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa;

(c) si zaidi ya wajumbe watano kutoka makundi maalum kama wazazi, vijana, wanawake, watu wenye ulemavu na wanafunzi watakaoteuliwa na Mkurugenzi husika wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

(d) si zaidi ya maofisa watatu kutoka katika Wizara watakaoteuliwa na Waziri; na

(e) si zaidi ya watu wazima watatu walioteuliwa na Waziri ambao wanaishi katika eneo hilo.

(2) Msaidizi Mkurugenzi anayehusika na sekta ya elimu katika Mamlaka husika ya Serikali za Mitaa atakuwa ni Katibu wa Bodi.

(3) Kazi, utaratibu na mambo mengine yanayohusiana na hayo chini ya kifungu hiki yatakuwa kama yatakavyoelezwa katika Kanuni".

Kuongezwa kifungu kipya cha 26C.

**27.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 26C mara baada ya kifungu cha 26B kama ifuatavyo:

"26C Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi na Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu, Nam. 10 ya 1996, na amri yoyote ya kiutawala, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kwa kuzihusisha na Misitu, zitakuwa na jukumu la jumla la usimamizi na uendeshaji Misitu ya Hifadhi ya Jamii".

Marekebisho ya kifungu cha 39.

**28.** Kifungu cha 39 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake kifungu kidogo cha (1) kipya kama ifuatavyo:

"(1) Kutakuwa na Mkurugenzi katika kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambaye atateuliwa na Rais".

Kuongezwa kifungu kipya cha 39A.

**29.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 39A mara baada ya kifungu cha 39 kama ifuatavyo:

"Wasaidizi Wakurugenzi.

39A. (1) Kutakuwa na Wasaidizi Wakurugenzi katika kila Mamlaka ya Serikali ya Mitaa ambao watateuliwa na Waziri.

(2) Wasaidizi Wakurugenzi watakuwa wasadizi wakuu wa Mkurugenzi na ndio watakaokuwa wakuu wa Idara kama zilivyoanzishwa katika kifungu cha 57 cha Sheria hii.

(3) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kama Msaidizi Mkurugenzi endapo atakuwa na:

(a) angalau shahada ya kwanza au inayolingana katika sekta husika;

(b) uzoefu wa kazi angalau miaka saba katika sekta husika; na

(c) kiwango cha juu cha uadilifu".

Marekebisho ya kifungu cha 41.

**30.** Kifungu cha 41 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza aya ya (f) mara baada ya aya ya (e) kama ifuatavyo:

"(f) Kuchukua hatua za kinidhamu kwa mtumishi yeyote wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma".

Marekebisho ya kifungu cha 42.

**31.** Kifungu cha 42 (2) cha Sheria Mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) katika aya (d):

(i) kufuta neno "watano" na kuweka badala yake neno "watatu";

(ii) kufuta maneno "Baraza la Wadi" na kuweka badala yake maneno "Mkuu wa Wilaya";

(iii) kufuta neno "watakaopendekezwa" na kuweka badala yake neno "watakaoteuliwa".

(b) katika aya (e):

(i) kufuta neno "watano" na kuweka badala yake neno "watatu";

(ii) kufuta maneno "Baraza la Wadi" na kuweka badala yake maneno "Mkuu wa Wilaya";

(iii) kufuta neno "watakaopendekezwa" na kuweka badala yake neno "watakaoteuliwa".

(c) katika aya (f):

(i) kufuta maneno "Baraza la Wadi" na kuweka badala yake maneno "Mkuu wa Wilaya";

(ii) kufuta maneno "na ambaye hatakuwa na haki ya kupiga kura". mwisho wa aya ya (f).

Marekebisho ya kifungu cha 43.

**32.** Kifungu cha 43 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta aya ya (f) ya kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake aya mpya ya (f) kama ifuatavyo:

"(f) kusimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi na programu za Halmashauri ya Wilaya ndani ya Wadi".

(b) kuongeza aya mpya ya (g) kama ifuatavyo:

"(g) kupanga na kuratibu shughuli na kutoa usaidizi na ushauri kwa wakaazi wa Wadi wanaofanya kazi au shughuli yoyote".

(c) Kuweka nambari upya aya ya (g) kuwa aya ya (h) kwa mpangilio wake.

Marekebisho ya kifungu cha 47.

**33.** Kifungu cha 47 cha Sheria Mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) katika aya ya (b) ya kifungu kidogo cha (2):

(i) kuongeza maneno "ambaye atateuliwa na Mkuu wa Wilaya" mwisho wa aya hiyo;

(ii) kufuta neno "watano" na kuweka badala yake neno "watatu".

(b) katika aya ya (d) ya kifungu kidogo cha (2):

(i) kufuta neno "watano" na kuweka badala yake neno "watatu";

(ii) kuongeza maneno "na kuthibitishwa na Mkuu wa Wilaya" mwisho wa aya hiyo.

(c) katika aya ya (e) ya kifungu kidogo cha (2):

(i) kufuta neno "watatu" na kuweka badala yake neno "wawili";

(ii) kufuta maneno "hana haki ya kupiga kura".

Marekebisho ya kifungu cha 57.

**34.** Kifungu cha 57 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (1) kama ifuatavyo:

"(1) Kutakuwa na idara ndani ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kama itakavyohitajika kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi zake kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma".

Marekebisho ya kifungu cha 70.

**35.** Kifungu cha 70 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongeza aya mpya za (viii), (ix) na (x) kama ifuatavyo:

(viii) kodi ya upangishaji;

(ix) mauzo ya mali zisizohamishika;

(x) faini zilizotozwa na Mahkama au thamani ya vitu vyote vilivyotaifishwa kwa amri ya Mahkama yoyote kwa uvunjwaji wa sharti chini ya Sheria hii au sheria ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

(b) kuzipa nambari upya aya (viii) kuwa (xi) kwa mpangilio wake.

Marekebisho ya kifungu cha 72.

**36.** Kifungu cha 72 kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (3) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (3) kama ifuatavyo:

"(3) Ruzuku yoyote iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, itatolewa kupitia Ofisa Mas-uli wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika moja kwa moja katika hesabu ya Benki ambapo matumizi yake yatawekewa utaratibu".

Marekebisho ya kifungu cha 75.

**37.** Kifungu cha 75 kinarekebishwa kwa:

(a) kuongezwa kifungu kidogo kipya cha (2) mara baada ya kifungu kidogo cha (1) kama ifuatavyo:

"(2) Mamlaka ya Serikali za Mitaa itatenga fedha kupitia bajeti yake kwa kusaidia vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kama itakavyoelekezwa na Waziri".

(b) kuvipa nambari upya vifungu vidogo vya (2), (3), (4), (5), (6) na (7) kuwa (3), (4), (5), (6), (7) na (8) kwa mpangilio wake.

Kuongezwa kifungu kipya cha 86A.

**38.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 86A mara baada ya kifungu cha 86 kama ifuatavyo:

"Uvunjaji wa majengo yasiyofaa.

86A. (1) Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika anaweza, kwa kushauriana na Mamlaka husika, kubomoa jengo lolote au sehemu ya jengo ambalo kwa maoni yake:

(a) limechakaa;

(b) lina kasoro za kiujenzi;

(c) limejengwa katika eneo la umma, eneo la wazi, njia au katika hifadhi yoyote ya barabara; au

(d) lipo katika hali ambayo kwa kufanyiwa matengenezo au marekebisho halitoweza kuondosha usumbufu.

(2) Mkurugenzi analazimika, kabla ya kufanya ubomoaji chini ya kifungu hiki, kumtumia indhari ya siku kumi na nne mmiliki wa jengo ili ahame kabla ya siku iliyotajwa katika indhari hiyo.

(3) Ikiwa mmiliki ameshindwa kufuata maelekezo yaliyomo katika indhari chini ya kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Laki Tano na atatakiwa kulipa gharama za ubomoaji".

Kuongezwa kifungu kipya cha 86B.

**39.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 86B mara baada ya kifungu cha 86A kama ifuatavyo:

"Taarifa ya maradhi ya kuambukiza.

86B. (1) Endapo mkaazi katika nyumba inayotumika kwa makaazi ameathirika na maradhi yoyote ya kuambukiza au dalili za maradhi hayo zinazopelekea maambukizi, masharti yafuatayo yatafuatwa:

(a) Mtumishi wa Afya au daktari atakayemuhudumia au kumtembelea mgonjwa atapaswa kutokana na kufahamu kuwa mgonjwa huyo ana maradhi ya kuambukiza au ana maradhi yanayoshukiwa kuambukiza, apeleke taarifa kwa muhudumu wa afya katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika ambayo itaeleza jina, jinsia ya mgojwa, mazingira ya jengo analoishi na chanzo cha maradhi hayo ambapo kwa maoni ya Afisa wa afya huyo, mtu huyo ameathirika au zipo dalili za kuwa ameathirika;

(b) Mgonjwa yeyote au jamaa wa karibu ambae ametambuliwa au anashukiwa kuathirika na maradhi yenye kuambukiza atajulishwa na Muhudumu wa Afya kuhusu jambo hilo na atalazimika kufuata maelekezo atakayopewa na hatua za kuchukua alizopewa na Mhudumu wa Afya;

(c) Mtumiaji au mmiliki wa jengo, pale atakapojua kuwa mgonjwa ameathirika kwa maradhi ya kuambukiza au anashukiwa kuwa na maradhi ya kuambukiza, atatoa taarifa kwa Afisa Dhamana

katika kituo cha afya kilicho karibu nae ambae Afisa huyo atamjuulisha Afisa Dhamana wa Afya wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika ambapo mtu huyo anaishi.

(2) Mtu yeyote anayepaswa chini ya kifungu hiki kupeleka indhari au cheti, ambaye atashindwa kufanya hivyo, atawajibika kulipa faini isiyopungua Shilingi Laki Tano au kutumikia kifungo cha muda wa miezi mitatu au vyote viwili".

Kuongezwa kifungu kipya cha 86C.

**40.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 86C mara baada ya kifungu cha 86B kama ifuatavyo:

"Kutii masharti ya Afya ya Jamii.

86C. Jengo lolote au eneo au sehemu ya jengo halitotumika hadi pale ambapo ithibati ya jengo hilo kukidhi vigezo vya kiafya imetolewa na Afisa wa Afya ya Jamii aliyeidhinishwa na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika". .

Marekebisho ya Jadweli la Kwanza.

**41**. Jadweli la Kwanza la Sheria Mama linarekebishwa kwa:

(a) kuongeza maneno "baada ya maelekezo kutoka kwa Waziri wa Afya" mwishoni mwa aya ya (b) ya kipengele cha 4;

(b) kuongeza maneno "baada ya kupata idhini kutoka kwa Waziri wa Elimu" mwishoni mwa aya ya (a) ya kipengele cha 5;

(c) kufuta maneno "miradi ya mashamba ya samaki" katika aya (k) ya kipengele cha 6 na kuweka badala yake maneno "ufugaji wa viumbe maji"; na

(d) kuongeza maneno "kwa Mamlaka husika" baina ya maneno "kutoa taarifa na "na" yaliyopo katika aya ya (m) ya kipengele cha 4.

## SEHEMU YA NANE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA (UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI) MAFUTA NA GESI ASILIA, NAM. 6 YA 2016

Kusomwa

**42.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya (Utafutaji na Uchimbaji) Mafuta na Gesi Asilia, Nam. 6 ya 2016, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 17.

**43.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 17 na kuweka badala yake kifungu **kipya** cha 17 kama ifuatavyo:

“Uteuzi wa Mkurugenzi Mwendeshaji.

17.(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Mamlaka atakayeteuliwa na Rais kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

(2) Mtu hatoteuliwa kuwa Mkurugenzi Mwendeshaji isipokuwa:

(a) awe Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza ya Chuo Kikuu katika fani ya mafuta na gesi asilia, ufundi, sheria, uchumi utawala wa umma au fani nyengine zozote zinazolingana na hizo kutoka Chuo kinachotambulika; na

(c) ana uzoefu wa kazi usiopungua miaka saba katika fani husika”.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 18 Juni, 2020.

..........................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***